**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**

**Mkuu wa Shule 0768661887**

**Makamu Mkuu wa Shule 0757912765**

**Matron 0753284724**

**Mwalimu malezi na nidhamu/patron 0759-912849**

**Shule ya Sekondari Mount Kipengere,**

**S.L.P 479,**

**Njombe.**

**14 June 2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MOUNT KIPENGERE HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………...

Shule ya Sekondari Mount Kipengere ipo umbali wa Kilometa 50 Magharibi ya Mkoa wa Njombe. Usafiri wa basi kutoka mji wa Njombe unapatikana katika kituo cha mabasi standi kuu Njombe. Mwanafunzi akishafika Njombe stendi apande mabasi yanayoelekea wilaya ya Makete au yanayoelekea Hospitali ya Ikonda na ateremke kijiji cha Kipengere. Nauli ni Shilingi 4,000/= kutoka Njombe hadi Kipengere. Usafiri wa kufika shule baada kuteremka kipengere pikipiki au boda boda ni Tsh.2000/=

Muhula wa Masomo utaanza tarehe **14/08/2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **20/08/2023**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

**A.WAVULANA**

- ✓ Mashati meupe mawili (02) mikono mirefu
- ✓ Suruali mbili ( rangi ya brown ya kuiva 1 na rangi ya blue bahahi 1)
- ✓ Tai (rangi ya blue bahar 1 na rangi ya brown ya kuiva i)
- ✓ Sweta moja kijani kibichi yenye shingo ya v
- ✓ Soksi nyeupe jozi mbili
- ✓ Nguo za kazi ( suruali nyeusi 01)
- ✓ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi pia vyenye kufunika miguu na viwe na kamba
- ✓ Vifaa vya michezo: truck suit 1 (sky blue) yenye mkanda mwepe na raba za michezo za ngozi jozi moja
- ✓ Jacket jeusi moja lisilo na kofia, wala maandishi yoyote au mchanganyiko wa rangi.

B. WASICHANA.

- ❖ Sketi 02 zinazofika kwenye magoti ( rangi ya brown ya kuiva na rangi ya blue bahari 01), mshono umeambatanishwa kwenye form.
- ❖ Suruali mbili ( rangi ya brown ya kuiva 01 na rangi ya blue bahari 01)
- ❖ Tai 2 ( rangi ya brown ya kuiva 01 na rangi ya blue bahari 01)
- ❖ Sweta 01 kijani kibichi yenye shingo ya **v**
- ❖ Soksi nyeupe jozi 02
- ❖ Nguo za kazi : (shamba dress 01) gauni yenye rangi ya damu ya mzee) iwe ndefu ya kufunika magoti
- ❖ Jacket jeusi moja lisilo na kofia, wala maandishi yoyote au mchanganyiko wa rangi.
- ❖ Wanafunzi kiislamu: hijabu nyeupe itavaliwa muda wa darasani na mtandio wa rangi ya pink, utavaliwa nje ya muda wa darasani.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counter books 10 quire 3 au 4
ii. **Ream (A4)** bunda moja na karatasi za kaki(rulled paper) bunda moja kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*;
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology pia aje na koti la kuvaa wakati wa masomo ya vitendo,liwe jeupe na liishie kwenye magoti muhimu sana.
v. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na uchumi;
vi. Godoro la size ya 21/2" x 6
vii. Mashuka Jozi 2 moja la blue jingine la pinki, blanket 1 zito, foronya ya godoro 1
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Ndala na vifaa vya usafi wake mwenyewe
xii. Tranker au sanduku la kuhifadhia vifaa vyake
xiii. Vifaa vya usafi vya jumla:
**HGK:** PANGA 1,SLASHER 1,JEMBE 1(MPINI WAKE), HARDA BLOOM 1,RUBBER SQUEEZER 1 NA UFAGIO WA CHELEWA 1
**CBG:** SLASHER 1,JEMBE 1,HARD BROOM 1,SOFT BLOOM 1,RUBBER SQUEZER 1 NA CHELEWA 1
**HGE:** SLASHER 1,JEMBE 1,HARD BLOOM 1,PANGA 1 NA KISHUNGI CHA KUSAFISHIA SINKI LA CHOO 1
**PCB:** PANGA 1,RUBBER SQUEZER 1,HARD BLOOM 1,SOFT BLOOM 1

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | 1ST AID | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote ilipwe kupitia akaunti ya SHULE 60601000017 NMB yenye jina la MOUNT KIPENGERE SEKONDARY COLLECTION REVENUE**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi**

**kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………**

**Jina la Mkuu wa Shule BELNOW B. MHANGA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- ➢ **Mkuu wa shule 0768-661-887**
- ➢ **Makamu Mkuu wa Shule 0757-912-765**
- ➢ **Mwandamizi Taaluma 0758-126-961**
- ➢ **Mwandamizi Malezi 0759-912-849**

**FORM Na F3. MEDICAL EXAMINATIONS**

(To be completed by medical officer)

1. Student's name…………………………………………………………………….
2. Age………………………………………………………………………………..
3. Blood count (white and red)…………………………………………………
4. Stool examination…………………………………………………………………..
5. Syphilis or/ and other venereal diseases test……………………………………….
6. T.B test………………………………………………………………….
7. Eye test…………………………………………………………………………………
8. Ears test…………………………………………………………………………………..
9. Abdomen…………………………………………………………………………………
10. Speen……………………………………………………………………………………..
11. Urine for plamo test……………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION

If any e.g physical defeats, impairment, infections, pregnancy, chronic or family diseases etc…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION

STATION…………………………………..Signature…………………………………..

Date…………………………………………Designation………………………………..

…………………………………………….

## FOMU YA KUKUBALI MASHARTI YA SHULE (F.1)

### A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi_________________________________kidato cha _______tahasusi________ Ninakubali kujiunga na shule ya sekondari Mount Kipengere nikiwa mwanafunzi wa bweni.
2. Ninakubali masharti yote na ninahidi kufuata sheria zote za shule.
3. Niko tayari uongozi wa shule kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa Pamoja na kunirudisha kwa mzazi/mlezi endapo nitakiuka masharti ya shule.
   Sahihi ya mwanafunzi_____________________tarehe_____________

### B. SEHEMU YA MZAZI

Mimi____________________________ninakubali mtoto wangu kujiunga na shule ya Sekondari Mount Kipengere kuanzia tarehe____________akiwa mwanafunzi wa bweni.

Ninakubali masharti yote yaliyomo katika maelezo ya kujiunga na shule ikiwa ni Pamoja na kulipa gharama za uharibifu wa mali za umma na kumtimizia mahitaji mengine ya shule. Nitakuwa tayari kumpokea mwanangu wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyomo au kubainika kuwa ana afya isiyoridhisha ambayo itahitaji ukaribu na matunzo ya mzazi / mlezi mwenyewe.

a) Anuani yangu ya kugumu ni:
   ____________________________________________
   ____________________________________________
   ____________________________________________

**FOMU YA MWANAFUNZI YA KUPOKELEWA SHULENI (F.2)**

1. Jina la mwanafunzi_____________________________________________
2. Mahali alipozaliwa_____________________________________________
3. Tarehe ya kuzaliwa_____________________________________________
4. Uraia___________________________________________
5. Anwani ya nyumbani_________________________________________
6. Anwani ya mzazi(kama tofauti na namba 5)________________________________
7. Jina la mzazi/ mlezi ____________________________________________________
8. Kazi ya mzazi/ mlezi_______________________________________________
9. Namba ya simu ya mzazi/mlezi_____________________________________
   Jaza taarifa za ndugu wengine watakaoweza kufika shule na kushughulikia masuala yote ya mwanao kwa muda wote awapo shuleni.

(a) Jina lake………………………..uhusiano…………………namba ya simu………………
(b) Jina lake………………………..uhusiano…………………namba ya simu………………
(c) Jina lake………………………..uhusiano…………………namba ya simu……………….
(d) Jina lake………………………..uhusiano…………………namba ya simu………………..

Picha (a) Picha (b) Picha (c) Picha (d)

Weka picha ya ndugu kwenye visanduku

Taamali: Ndugu walioandikwa ndio wanapaswa kushughulikia masuala ya nidhamu, maendeleo na uhamisho wa mwanafunzi husika tu. Iwapo kutatokea mabadiliko kwa sababu yoyote ile, taarifa iletwe shuleni ili kufanyike mabadiliko.

10.dini………………………………………………………..

11.kidato ulichopokelewa…………………

12.Tahasusi ( combination)………………………………

13.Shule uliyotoka …………………………………

14. Shughuli unazozipendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, ridhaa, kuimba n.k

15. Wilaya unayotoka………………….Mtaa………………..Kata……………………….

16. Sahihi ya mwanafunzi………………………………Tarehe…………………

17. Sahihi ya Mzazi……………………………Tarehe……………………………..

## FOMU NA. 4

PLEAS, IF POSSIBLE, COME WITH THE FOLLOWING BOOKS/ REFERENCE MATERIALS RELEVANT TO YOUR COMBINATION AS LISTED BELLOW: -

1.HISTORY

i) Major Events in African History

ii) The political, Economy and emperialismL

iii) Africa Since 1800 -4th Edition

iv) The making of modern Africa

v) How Europe underdeveloped Africa

vi) The 20th Century

2. GEOGRAPHY

i) Certificate of Geography ( Oxford)

ii) General Geography in diagrams

iii) Photograph interpretation and elementary surveying for secondary level

iv) Regional Geography

v) Certificate Human and Economic Geography

3. CHEMISTRY

i) Physical chemistry for A-level

ii) Inorganic chemistry ( party A and B)

iii) Organic Chemistry ( party A and B)

iv) Chemistry in Action

4.BIOLOGY

i) biological science

ii) Biology ( guide to dissection)

iii) Dissecting Kit ( kila mwanafunzi awe nayo)

5.GENERAL STUDIES

i) Understanding Advanced level General studies

ii) General studies notes (V & VI)

6.KISWAHILI

USHAIRI

i)kimbunga---- H.Gora

ii) Chungu Tamu----T. Mvungi

iii) Mapenzi Bora -----MS. Khatibu

RIWAYA

i)Vuta N'kuvute -----Shafi A. Shafi

ii)Kufikirika -----------S. Robert

iii) Mfadhili………..Hussein Tuwa

iv) Usiku Utakapo kwisha………..Mbunda msokile

TAMTHILIYA

i)Morani……….E.Mbogo

ii)Kivuli Kinaishi……..S. Mohamed

iii)Kwenye Ukingo wa Thim………..E. Hussein

iv) Nguzo mama………(DUP)1982

7.PHYSICS

i)Physics Book by S Chand I & II

ii) Physics Book by Tom Dancan

iii) Physics Book by Roger Manchester

iv) Principle of Physics by Nelkon

8. ECONOMICS

i)Modern Economics by Mudida

ii) Economics simplified by saleen

iii) Principle of Economics by Ahuja

iv) Postive Economics 8th Edition By Lipsey

v) Introduction to Economics Theory by Gupta

## MUUNDO WA VAZI LA MWANAFUNZI WA KIKE

NB. Sketi lazima ifike kwenye magoti.

